TANGAZO LA SERIKALI Na. 216 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA HOSPITALI KITANGARI YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Hospitali Kitangari ya Mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

*GN. NO. 216 (Contd.)*

______

JEDWALI

______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H1 yenye majira - nukta 538914MS, 8821708KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $40^0$ 15'48'' kwa umbali wa kilomita 0.657 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H2 yenye majira - nukta 537589MS, 8821207KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata barabara ya Mtopwa-Kitangari hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H3 yenye majira - nukta 536517MS, 8821938KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $11^0$ 23'43'' kwa umbali wa kilomita 0.139 hadi kwenye alama ya mpaka ya upiamji namba H4 yenye majira - nukta 536544MS, 8822074KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $65^0$ 07'24'' kwa umbali wa kilomita 0.417 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H5 yenye majira - nukta 536923MS, 8822250KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $14^0$ 27'18'' kwa kilomita 0.492 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H6 yenye majira - nukta 536800MS, 8822726KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $67^0$ 06'59'' kwa umbali wa kilomita 0.176 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H7 yenye majira - nukta 536637MS, 8822795KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $16^0$ 27'36'' kwa umbali wa kilomita 0.146 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H8 yenye majira - nukta 536596MS, 8822935KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $75^0$ 13'51'' kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H9 yenye majira - nukta 536712MS, 8822966KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $42^0$ 42'34'' kwa umbali wa kilomita 0.112 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H10 yenye majira - nukta 536789MS, 8822883KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $88^0$ 04'10'' kwa umbali wa kilomita 0.565 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H11 yenye majira - nukta 537354MS, 882286KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $41^0$ 55'14'' kwa umbali wa kilomita 0.693 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H12 yenye majira - nukta 537817MS, 8822348KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $17^0$ 06'40'' kwa umbali wa kilomita 0.669 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*